Ambacho Dhambi Ndogondogo Hufanya
(What Little Sins Do)

na

Ellis P. Forsman

Ambacho Dhambi Ndogondogo Hufanya
(What Little Sins Do)

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 17, 2011

Ambacho Dhambi Ndogondogo Hufanya

Mit. 6:6-11

Kuna vitu vingi vidogovidog katika dunia hii ambazo tunaweza kujifunza kwayo.

Angalia chungu.

Mit. 6:6-11, "*Ewe mwendee chungu, zitafakari njia zake upate hekima. Kwa maana yeye hana akida, wala msimamizi wala mkuu, lakini hujiwekea hakiba ya chakula wakati wa jua; hukusanya chakula chake wakati wa mavuno. Ewe mvivu utalala hata lini? Utaondoka lini katika uzingizi wako? Bado kulala kidogo kusinzia kidogo, bado kunja mikono upate usingizi! Hivyo umaskini wako huja kama mnyang'anyi, na uhitaji wako kama mtu mwenye silaha.*"

Ni mdogo sana; akichukuliwa kwamba hafai.

Watu wanataka kuzuia mauaji ya paa, uwindaji, punda, mbwa, n.k.

Mungu mara nyingi amewaambia watu wake kuwaua wanyama, ambazo ziliwekwa hapa kwa ajili ya binadamu. Mwanzo 1:28-30, "*Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi. Mungu akasema tazama nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya nchi yote pia, na kila mti ambao matunda yake yana mbegu; vitakuwa ndivyo chakula chenu; na chakula cha kila mnyama wan chi, na cha kila ndege wa angani, na cha kila kitu kitambaacho juu ya nchi, chenye uhai; majani yote ya miche, ndiyo chakula chenu ikawa ivyo.*"

Hataivyo, watu hawahawa ambao husema kuwa mauaji ya wanyama ni vibaya hawafikiri chochote kuhusu kula kuku au hambaga, au mauaji ya panya, kumkanyaga chungu au buibui, au kumpiga nzi au mbu.

Wanadhani kwamba hivi ni vidogo na havijalishi.

Leo, kuna kasumba ya "konyeza" dhambi

Wengine wanapenda kuiita tatizo la "ubinafsi", badala ya kuiita dhambi. Wengine husema, "Usiwe na akili ndogo" au "Hicho ni kitu kidogo." Tuna sikia kuhusu dhambi "ndogo" na dhambi "kubwa", "uongo mweupe". "nusu ya ukweli", "Vidole vyangu vili zungukwa."

Kweli, baadhi ya dhambi huchukua madhara madogo katika maisha haya; hii haimanishi, hataivyo, kwamba Mungu anaangalia dhambi moja tofauti na jinsi anayoiangalia nyingine.

Tunapaswa kuitazama dhambi kama Mungu anavyoitazama

- Siyo ya kiungu (kinyume na Mungu Mtakatifu).
- Mbaya (siwezi kufikiria jinsi ilivyo mbovu).
- Inauwa (huangamiza kwa wakati na milele).

Mungu anaitazamaje dhambi?

Habakuki 1:13, "*Wewe uliye na macho safi hata usiweze kuangalia uovu, wewe usiyeweza kutazama ukaidi, mbona unawaangalia watendao kwa hila; na kunyamaza kimya hapo mtu mwovu ammezapo mtu aliye mwenye haki kuliko yeye.*"

Hupaswi hata kuutazama uovu.

Angalia baadhi ya madhara ya kile kinachoitwa dhambi "ndogo"

Nzi wadogo wanaweza kuharibu.

Vitu vidogo virukavyo uharibu.

Mhu. 10:1, "*Mainzi mafu huvundisha marhamu ya mwuza marashi; kadhalika upumbavu haba ni mzito kuliko hekima na heshima.*"

Nzi wadogo wafu husababisha aroma ya dhihaka kwa kitu kilichokusudiwa kunukia vizuri. Nzi mdogo mfu anaweza kuharibu chakula.

Nidhamu ndogo humuaribu mtu ambaye anachukuliwa kama mwenye hekima na kuheshimiwa. Anapoteza mvuto wake nzuri.

Utundu wenye dhihaka?

Mbweha wadogo uharibu uzao wa mzabibu.

Wimbo wa Sulemani 2:15, "*Tukamatie mbeha, wale mbweha wadogo, waiharibuo mizabibu, maana mizabibu yetu yachanua.*"

Sielewi kiuhalisia uharibifu ambao mbeha hufanya, kuliko kula mizabibu, lakini inaonekana pia wanaharibu shina la mzabibu.

Funza mdogo kwenye kabechi anaweza kuharibu kabechi nzima kwa ajili ya biashara.

Vitu vidogo vinaweza kukua katika vitu vikubwa.

Kuchachua.

1 Kor. 5:6-7, "*Kujisifu kwenu si kuzuri. Hamjui ya kwamba chachu kidogo hulichachusha donge zima? Basi jisafisheni, mkatoe ile chachu ya kale, mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo hamkutiwa chachu. Kwa maana Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka, yaani Kristo.*"

Amira huifanya mkate kukua kwa haraka.

Jiwe dogo husababisha mikwaruzo kuenea katika kisima.

Mwiba unaweza kuangamiza sehemu kubwa.

Miaka kadhaa, hakukua na mwiba hata mmoja katika Australia yote. Mskochi , ambaye aliitamani miba, akafikiria kuwa ni vibaya kwamba eneo kubwa hilo lote liwe bila mmea. Hivyo akaweka mbegu ya mwiba kwenye kifungashio, na kuituma kwa mmoja wa maraffiki zake huko Australia. Sasa ilipofika, afisa mmoja wa forodha angesema, "Oh ilete ndani; je hilo siyo jiwe dogo? Inapaswa tu kutupwa shambani." Ndiyo, ilikuwa ndogo lakini; lakini sasa wilaya zote za nchi imezungukwa nayo na imekuwa mdudu wa wakulima na pigo. Ilikuwa ndogo, lakini ikaja kuwa adha kubwa. Jichunge na mbegu ya mwiba; dhambi ndogo inafanana nayo. (Nashangaa kama alikuwa ni uyu huyu Mskochi aliyeleta Mfagio wa Kiskotchi katika kaskazini mashariki mwa Amerika?).

Kitu kidogo kilisababisha anguko la mwanadamu

Tunda lililokataliwa katika Bustani ya Edeni.

Uongo "mdogo" wa shetani: "*Hakika hamtakufa.*"

Matokeo ya hiyo dhambi "ndogo" ilikuwa ni kifo.

- Rum. 5:14, "*Walakini mauti ilitawala tangu Adamu mpaka Musa, nayo iliwatawala hata hao wasiofanya dhambi ifananayo na kosa la Adamu aliyemfano wake yeye atakayekuja.*"
- 1 Kor. 15:22, "*Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa.*"

Kutaka kuwa na wengi motoni kwa sababu ya dhambi "ndogo."

Hii inaweza kuanzisha umuhimu wa kumtii Mungu.

Wengi katika Biblia walihukumiwa kwa sababu ya dhambi "ndogo"

Nadabu na Abihu.

Law. 10:1-2, 10, "*Nadabu na Abihu wana wa Haruni, wakatwaa kila mtu chetezo chake, wakatia moto ndani yake, wakatia na uvumba, nao wakatoa moto wa kigeni mbele ya BWANA, ambao yeye hakuwaagiza. Kisha moto ukatoka hapo mbele za BWANA, nao ukawala, nao wakafa mbele za BWANA. … Kisha mpate kupambanua kati ya yaliyo matakatifu na hayo yaliyo ya siku zote, na kati ya yaliyo najisi na hayo yaliyo safi;*"

"Baada ya yote, moto ni moto."

Waliangamizwa kwa dhambi yao "ndogo".

Uza.

2 Sam. 6:3-4, 6-7, "*Wakaliweka sanduku la Mungu juu ya gari jipya wakalitoa katika nyumba ya Abinadabu, iliyoko kilimani; nao Uza na Ahio wana wa Abinadabu wakaliendesha lile gari jipya. Wakalitoa katika nyumba ya Abinadabu iliyoko kilimani pamoja na sanduku la BWANA; na huyo Ahio akatangulia mbele ya sanduku. … Hata walipofika kwa uga ya Nakoni, Uza akalivyoshea mkono sanduku la Mungu akalikamata kwa maana wale ng'ombe walikunguwaa. Ndipo hasira ya BWANA ikawaka juu ya Uza; naye Mungu akampiga huko kwa kosa lake; hata akafa pale pale penye sanduku la Mungu.*"

Uza alilishika sanduku na akafa.

Haikuwa tendo baya.

Wengi wanaweza kuliona tendo hili la kulishika sanduku kama kitu "kidogo".

Akani.

Yoshua 7:1-26, "*Lakini wana wa Israeli walifanya dhambi katika kitu kilichowekwa wakfu; maana Akani mwana wa Karmi, mwana wa Zabdi, mwana wa Zera, wa kabila ya Yuda, alitwaa baadhi ya vitu vilivyowekwa wakfu; hasira ya BWANA ikawaka juu ya wana wa Israeli. Kisha Yoshua akatuma watu kutoka Yeriko mpaka mji wa Ai, ulio karibu na Bethaveni, upande wa mashariki wa Betheli, akawaambia akisema, pandeni juu mkaipeleleze nchi, basi wakapanda juu wakaupeleleza Ai. Wakarejea kwa Yoshua wakamwambia, wasiende watu wote, ila waende kama watu elfu mbili, tatu, wakaupige Ai; usiwataabishe watu wote kwa kuwaendesha huko; maana watu hao ni wachache tu. Basi watu wakaenda huko wapata elfu tatu tu; nao wakakimbia mbele ya watu wa Ai. Watu wa Ai wakawapiga watu kama thelathini na sita; wakawafuatia*

kutoka mbele ya mlango mpaka Shebarimu, wakawapiga huko kwenye matelemko; mioyo ya watu ikayeyuka ikawa kama maji. Yoshua akararua mavazi yake, akaanguka kifudifudi mbele ya sanduku la BWANA hata jioni, yeye na wazee wa Israeli wakatia mavumbi vichwani mwao. Yoshua akasema Ee Bwana MUNGU, kwa nini umewavusha watu hawa mto wa Yordani, ili kututia katika mikono ya Waamori, na kutuangamiza? Laity tungelikuwa radhi kukaa ng'ambo ya Yordani. Ee Bwana niseme nini baada ya Israeli kuwapa visogo adui zao? Maana Wakaanani na wenyeji wote wan chi hii watasikia habari hii, nao watatuzingira, na kulifuta jina letu katika nchi. Nawe utafanya nini kwa ajili ya jina lako kuu? BWANA akamwambia Yoshua, haya inuka, mbona umeanguka kifudifudi hivi? Israeli wamefanya dhambi, naam, wamelivunja agano langu nililowaagiza; naam, wametwaa baadhi ya vitu vilivyowekwa wakfu; tena wameiba, tena wameficha na kuvitia pamoja na vitu vyao wenyewe. Ndiposa wana wa Israeli hawawezi kusimama mbele ya adui zao, wakawapa visogo adui zao, kwa sababu wamelaaniwa; mimi sitakuwa pamoja nanyi tena; msipokiharibu kitu kile mlicho nacho kilicho wekwa wakfu. Haya inuka, uwatakase watu ukaseme, Jitakaseni, mwe tayari kesho; maana BWANA Mungu wa Israeli asema hivi; kitu kilichowekwa wakfu kiko katikati yako, Ee Israeli; huwezi kusimama mbele ya adui zako, hata mtakapo kiondoa kile mlichonacho, kilichowekwa wakfu. Basi asubuhi mtaletwa karibu nami kabila kwa kabila; kisha itakuwa ya kwamba kabila ile atakayoitwaa BWANA itakaribia jamaa kwa jamaa; na jamaa ile atakayoitwaa BWANA itakaribia nyumba kwa nyumba; na nyumba ile atakayoitwaa BWANA, itakaribia mtu kwa mtu. Tena itakuwa ya kwamba yeye atakayetwaliwa, naye anacho kitu kile kilichowekwa wakfu, atateketezwa kwa moto, yeye vitu vyote alivyo navyo; kwa sababu amelivunja agano la BWANA, na kwa sababu ametenda upumbavu katika Israeli. Basi Yoshua akaondoka asubuhi na mapema akawasogeza Israeli kabila kwa kabila, ; kabila la Yuda iakatwaliwa. Akazisogeza jamaa za Yuda, akaitwaa jamaa ya Wazera; akaisogeza jamaa yaWazera, mtu kwa mtu; Zabdi akatwaliwa. Akawasogeza watu wa nyumba yake mmoja mmoja; na Akani mwana wa Karmi, mwana wa Zabdi, mwana wa Zera, wa kabila ya Yuda akatwaliwa. Yoshua akamwambia Akani, mwanangu nakusihi, umtukuze BWANA Mungu wa Israeli, ukaungame kwake; uniambie sasa ulilolitenda; usinifiche. Akani akamjibu Yoshua, akasema kweli nimefanya dhambi juu ya BWANA Mungu wa Israeli nami nimefanya mambo haya na haya. nilipoona katika nyara joho nzuri ya Babeli, na shekel mia mbili za fedha, na kabari ya dhahabu, uzani wake shekeli hamsini, basi nalivitamani nikavitwaa; tazama vimefichwa mchangani katikati ya hema yangu na ile fedha chini yake. Wakavitoa kutoka hapo katikati ya hema, wakavileta kwa Yoshua, na kwa wana wa Israeli wote, nao wakaviweka chini mbele za BWANA. kisha Yoshua na Israeli wote pamoja naye, wakamtwaa Akani mwana wa Zera na ile fedha

na lile joho, na ile kabari ya dhahabu, na mawe, na binti zake, na ng'ombe zake, na punda zake, na kondoo zake, na hema yake, na vitu vyote alivyokuwa nanvyo, wakavileta juu hata bonde la Akori. Yoshua akasema mbona umetufadhaisha hivi? BWANA atakufadhaisha wewe leo. Ndipo Israeli wote wakampiga kwa mawe, kisha wakawateketeza kwa moto na kuwapiga kwa mawe. Kisha wakakusanya juu yake chungu kubwa ya mawe hata leo; naye BWANA akauacha ukali wa hasira yake. Kwa sababu hiyo jina la mahali pale likaitwa, Bonde la Akori, hata ivi leo."

Ubaya ulikuwa wapi kuchukua vifaa vya kivita? Hakukuwa na ubaya, wengi wanaweza kujibu.

Akani alikuwa na wazo hili.

Dhambi yake "ndogo" iligharimu siyo tu maisha yake, bali pia na maisha ya familia yake. Hakuna aliyepaswa kuchukua kitu katika mji wa Yeriko ulioangamizwa; lakini Akani alichukua baadhi ya vitu vilivyowekwa wakfu na kuvificha chini ya mchanga katika hema lake. Wote walipigwa mawe wakafa.

Anania na Safira.

Mdo. 5:1-6, "*Lakini mtu mmoja jina lake Anania, pamoja na Safira mkewe, aliuza mali, akazuia kwa siri sehemu ya thamani yake, mkewe naye akijua haya, akaleta fungu moja akaliweka miguuni pa mitume. Petro akasema Anania kwa nini shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu, na kuzuia kwa siri sehemu ya thamani ya kiwanja? Kilipokuwa kwako hakikuwa mali yako? Na kilipokuwa kimekwisha kuuzwa, thamani yake hakikuwa katika uwezo wako? Ilikuwaje hata ukaweka neno hili moyoni mwako? Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu. Anania aliposikia maneno haya akaanguka, akafa. Hofu nyingi ikawapata watu wote waliosikia haya. vijana wakaondoka, wakamtia katika sanda, wakamchukua nje wakamzika.*"

Walidhani ni dhambi "ndogo" na uongo au udaanganyifu ulikuwa sawa.

Walimdanganya Mungu.

Kile ambacho dhambi "ndogo" hufanya leo

Katika ulimwengu wa kibiashara.

Kuna uaminifu mdogo kwa watu wengi, lakini watu wengi hawaendi mbinguni.

"Dhambi ndogo" uliwapeleka watoza ushuru gerezani; biashara ya umasikini"; wengine wamepoteza kazi zao kwa ajili ya dhambi ndogo; zinasababisha aibu na dhihaka.

Katika ndoa.

Wengine husema, kutokuwa waaminifu kidogo unategemewa katika ndoa nyingi."

Inasababisha talaka na miji kuvunjika; inawaacha watoto bila wazazi; inaacha mioyo iliyovunjika na kutesa maisha.

Kile ambacho dhambi "ndogo" hufanya katika umilele

Zinasababisha mauti ya pili (kutengwa na Mungu milele).

Isa. 59:1-8, "*Tazama mkono wa BWANA haukupunguka, hata usiweze kuwaokoa wala sikio lake si zito, hata lisiweze kusikia; lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata hataki kusikia. Kwa maana mikono yenu imetiwa unajisi kwa damu, na vidole vyenu vimetiwa unajisi kwa uovu; midomo yenu imenena uongo, ndimi zenu zimenong'ona ubaya. Hapana adaiye kwa haki, wala hapana atetaye kwa kweli; hutumainia ubatili, hunena uongo, hupata mimba ya madhara, na kuzaa uovu. Huangua mayai ya fira, na kusuka wavu wa buibui; yeye alaye mayai yao hufa na hilo livunjwalo hutoka nyoka. Nyavu zao hazitakuwa mavazi, wala hawatajifunika kwa kazi zao kazi zao ni kazi za uovu, na vitendo vya udhalimu vimo mikononi mwao. Miguu yao hukimbilia mabaya, nao hufanya haraka kumwaga damu isiyo na hatia; mawazo yao ni mawazo ya uovu; ukiwa na uharibifu zaonekana katika njia kuu zao. Njia ya amani hawaijui; wala hapana hukumu yaa haki katika miendo yao; wamejifanyizia njia zilizopotoka; kila apitaye katika njia hizo hajui amani.*"

Mungu hasikilizi maombi ya wenye dhambi. Tubu.

Zinasababisha adhabu ya milele.

Ufu. 21:8, "*Bali waoga na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili.*"

Zinasababisha umilele pamoja na wasiomcha Mungu wa vizazi vyote.

Hii inapaswa kuonyesha jinsi dhambi "ndogo" hakika zilivyo.

Hitimisho

Usiruhusu dhambi “ndogo” itawale hatima yako.

Yak. 3:4-6, “*Tena angalieni merikebu; ingawa ni kubwa kama nini na kuchukuliwa na pepo kali, zageuzwa na usukani mdogo sana, kokote anakoazimia kwenda nahodha. Vivyo hivyo ulimi nao ni kiungo kidogo, nao hujivuna majivuno makuu. Angalieni jinsi moto mdogo uwashavyo msitu mkubwa sana. Nao ulimi ni moto ule ulimwengu wa uovu, ule ulimi umewekwa katika viungo vyetu, nao ndio uutiao wmili wote unajisi, huuwasha moto mfulizo wa maumbile, nao huwashwa moto na jehanam.*”

Lazima tuachane na wazo la dhambi “ndogo.”

Dhambi zote ni mbaya, na zitakutupa nje.

Kama una hatia ya dhambi “ndogo”, unapaswa kutambua madhara yake, na utubu – fanya juhudi za kweli kutokuendelea nazo.

“Vitu vikubwa katika maisha yanaonyesha sisi ni wakina nani. Vitu vidogo katika maisha vinaonyesha sisi tukoje!” (Chanzo hakijulikani.)

Maisha mara zote hurukia vitu vidogo.